

**Namba za simu.**

MKUU WA SHULE 0756331303

MAKAMU MKUU WA SHULE 0787542991

Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi .....

S.L.P .....

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ISSUNA WILAYA YA  
IKUNGI MKOA WA SINGIDA MWAKA 2021.**

**1.0 Utangulizi.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari **Issuna** ipo umbali wa **kilomita 27** kusini mashariki mwa halmashauri ya wilaya ya **Ikungi**.

Usafiri wa basi kutoka mjini **Singida** unapatikana katika kituo cha mabasi **Singida** nauli ni Tsh4,000/= Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021**. Ndani ya siku saba.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.**

**2.1 Sare za shule.**

- a) Sare ya shule hii ni **suruali rangi ya damu ya mzee yenye marinda mawili na pindo kwa chini na mkanda wa ngozi mweusi usiokuwa na chuma kubwa la kufungia** kwa wavulana, kwa wasichana **sketi mbili za rangi ya damu ya mzee**. mshono wa **marinda box sita (six boxes)** yanayolingana yaani mbele matatu na nyuma matatu.
- b) Shati rangi nyeupe mikono mifupi (Tomato) pamoja na sweta rangi ya damu ya mzee.
- c) Sketi rangi nyeusi ya kushindia na T-shirt yenye kola rangi ya blue ya shule kwa wanafunzi wa hostel.
- d) Mashuka mawili rangi yoyote, na bed cover rangi ya Pink zain (tetron pink zain) kwa hostel.
- e) Tshirt ya rangi ya dhahabu, viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na soksi nyeupe kwa wavulana na wasichana. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kuvaliwa shuleni ( kwa wale wa hostel aje na kanga au vitenge pea moja au zaidi na taulo.
- f) Rangi ya hijabu kwa waislamu ni kitambaa cheupe.(kijuba cheupe na sketi au suruali ya damu ya mzee)
- g) Sare ya michezo kwa shule hii ni **track suit rangi ya maji bahari (light blue)** kwa wavulana na wasichana.

**2.2** Aje na daftari (counter book 10), kalamu 10, mkebe wa hesabu na begi la kubebea madaftari yake. Vitu vyote hivi vitakaguliwa na mkuu wa shule mara tu atakaporipoti shuleni.

**2.3** Wazazi watagharamia chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

**2.4** Wazazi wa wanafunzi wa hostel watagharamia gharama za hostel jumla ya Tshs **540,000/=** kwa mwaka, fedha hizo zitalipwa kwa nusu muhula Tshs **270,000/=** Lipa kwenye Kamati ya hostel shuleni.

**2.5** Wazazi wa wanafunzi wa hostel watagharamia nauli ya wanafunzi kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Vitu vingine atakavyo gharamia mzazi ni **godoro ft mbili na nusu kwa sita, mto, mashuka matatu, mawili rangi ya maji bahari (light blue)** na moja **rangi nyeupe. sahani, kikombe, kijiko, ndoo ndogo mbili, tranker na fedha ya matumizi binafsi (pocket money).**

### **3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule.**

Mwanafunzi utatakiwa kufuata sheria zifuatazo.

#### **A. NIDHAMU.**

- a) Kuheshimu walimu wote, watumishi wengine pamoja na wanafunzi wenzako uwapo ndani na nje ya shule.
- b) Kuheshimu bendera ya taifa na nembo zote za taifa.
- c) Kushirikiana na wanafunzi wengine katika masomo na shughuli zingine.
- d) Kuvaa mavazi ya heshima muda wote uwapo shule na nje ya shule.
- e) kutunza mali zote za umma.
- f) Kuwa mvumilivu
- g) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na zishonwe kulingana na maelekezo.

#### **B. MAHUDHURIO.**

- a) Kufuata ratiba ya shule kikamilifu.
- b) Kuhudhuria darasani siku zote za masomo.
- c) Kufika kwa wakati pale unapohitajika.
- d) Utatakiwa kuhudhuria pared kulingana na ratiba ya shule.

### **3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa shule.**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nakadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau bendera ya Taifa.
- h) Kuoa au kuolewa.
- i) Kuwa mjamzito / Kutoa mimba / kusababisha mimba.
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- l) Kuwa na simu ya mkononi.

- 4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**
- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikari. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
  - b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
  - c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- 5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

*Thomas*

SELESTINA B. THOMAS.

MKUU WA SHULE.

HEADMISTRESS  
ISSUNA SECONDARY SCHOOL  
P.O. BOX 440-SINGIDA

Mzazi/Mlezi Wa Mwanafunzi.....

**YAH: KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE  
YATAKAYOTOLEWA NA SHULE PIA KUSHIRIKIANA NA SHULE KUMLEA  
MWANAFUNZI.**

**4.0 Taarifa binafsi za mwanafunzi.**

- a) Jina kamili.....
- b) Tarehe ya kuzaliwa.....
- c) Dini.....dhehebu.....
- d) Anwani kamili ya nyumbani ambapo mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo.....

**Uthibitisho wa mwanafunzi.**

Mimi..... nimesoma barua ya kuripoti shuleni, sheria za shule , nimeelewa na kuridhika na ninakubali endapo nitaenda kinyume na maelekezo hayo hatua za kinidhamu zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina la mwanafunzi.....sahihi.....tarehe.....

**4.1 Taarifa binafsi za mzazi/ mlezi.**

- a) Jina kamili.....
- b) Yeye ni mzazi au mlezi.....
- c) Uhusiano uliopo.....
- d) Kazi yake.....
- e) Anwani yake.....namba ya simu.....

**Uthibitisho wa mzazi.**

Mimi..... Naahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na walimu katika kumlea kijana wangu ili awe na tabia njema siku zote, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo. Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule. Juu ya hayo naelewa mwanangu akienda kinyume na sheria za shule hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina la mzazi/mlezi.....sahihi.....tarehe.....